JARIDA LA

# AZANIAFRONT CATHEDRAL

www.azaniafront.org

KKKT AZANIAFRONT CATHEDRAL

Jarida #008 Januari - Machi 2020



03 FARAGHA YA WAZEE WA BARAZA BAGAMOYO YAFANA, WAPENDEKEZA IFANYIKE MARA KWA MARA

07 WANAWAKE WAFANYA IBADA YA MAOMBI YA SHUKRANI

05 AZANIAFRONT YAADHIMISHA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

11 WANAWAKE WAONGOZA IBADA YA KWARESMA

**Salaam za Mchungaji Kiongozi,**

**Charles Mzinga**

Bwana asifiwe washarika, ni fursa nyingine adimu ya kujikumbusha na kupeana taarifa juu ya mambo mbalimbali yanayoendelea hapa usharikani kwetu Azaniafront na kanisa zima kwa ujumla.

Ikiwa tunamaliza robo ya kwanza ya mwaka 2020, shughuli mbalimbali zimeweza kufanyika hapa usharikani katika kipindi hiki cha miezi mitatu kama ambavyo utapata fursa ya kuzisoma kwa kina ndani ya toleo hili la Kijarida. Pia niwakumbushe washarika kutembelea tovuti rasmi ya usharika ambayo ni **www.azaniafront.org** ili kupata taarifa na matukio mbalimbali yanayohusu usharika wetu.

Ili kurahisisha mawasiliano baina yetu, kila kikundi hapa usharikani kina group la WhatsApp, niwaombe washarika wote muweze kutumia magroup hayo kwa malengo yaliyokusudiwa ili kuweza kufikishiana taarifa muhimu zinazohusu usharika wetu. Hii itatusaidia kukaa tukiwa wamoja na rahisi kufamishana jambo kwa haraka pale inapobidi.

Pia, natoa pongezi za dhati kwa washarika wote kwa kuendelea kutoa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa kazi na mipango mbalimbali ya usharika, lakini pia kwa kujitolea kusaidia jamii zinazokuwa na uhitaji kama watoto yatima, wazee pamoja na wagonjwa.

Kuhusu janga la Virusi vya Corona (COVID-19) linaloitesa dunia kwa sasa, niwaombe washarika kuendelea kuchukua tahadhari na kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya ili kujikinga na maambukizi ya virusi hivyo hatari. Taarifa kwa kina na hatua ambazo usharika umechukua katika kupambana na janga hili zinapatikana katika ukurasa wa pili wa kijarida hiki. Kama uongozi wa usharika, ni jukumu letu kuhakikisha afya za washarika wote zinakuwa katika hali ya usalama.

Tuendelee kumwomba na kumtumikia Mungu wetu ili atuepushe na majanga ya aina mbalimbali. Pia, tuendelee kujitolea kusaidia watu wengine wenye uhitaji pale inapobidi maana kwa kufanya hivyo tunamtukuza Bwana wetu aliye hai.

***Mungu awabariki wote..!***

# Tuchukue tahadhari kujikinga na COVID-19

**Na Paulin Paul**

Tangu mwezi Disemba mwaka 2019, dunia imekuwa katika hali ya taharuki ikijaribu kupambana na mlipuko wa virusi vya Corona (COVID-19), ugonjwa ambao, kwa mujibu wa Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO), ulianzia katika jimbo la Wuhan nchini China kabla ya kusambaa katika maeneo mengine ya dunia ikiwemo nchini Tanzania.

Jitihada mbalimbali zimekuwa zikifanywa na jumuiya ya kimataifa, taasisi binafsi pamoja na serikali za mataifa mbalimbali ili kupunguza au kutokomeza kabisa maambukizi ya virusi hivyo ambavyo vimeonekana kuwa tishio kwa maisha ya binadamu kiasi cha WHO kuitangaza COVID -19 kama janga la ulimwengu.

Nchini Tanzania, Wizara ya Afya imekuwa ikitoa miongozo mbalimbali kwa wananchi juu ya namna bora ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya Corona pamoja na kutoa huduma stahiki kwa ambao wamethibitika kukutwa na virusi hivyo baada ya kufanyiwa vipimo.

Shughuli mbalimbali za kibinadamu (kijamii na kiuchumi) zimeweza kuathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na kusambaa kwa virusi vya Corona. Kwa mujibu wa WHO, tahadhari ya kwanza ya kukabiliana na kusambaa kwa kasi kwa virusi hivyo ni kupunguza misongomano ya watu pamoja na kunawa mikono mara kwa mara kwa kutumia dawa maalumu za kuua vijidudu (sanitizer).

Kwa upande wa kanisa, Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront umekuwa mstari wa mbele katika kuunga mkono juhudi za serikali za kupambana na maambukizi mapya ya virusi vya Corona kwa kutoa elimu juu ya namna bora ya kujikinga kwa washarika kila siku za Jumapili katika ibada zote. Pia usharika uliweka vifaa maalumu vya kunawa mikono katika kila mlango wa kuingia kanisani pamoja na ofisi za usharika ili watu wote wanaoingia na kutoka katika mazingira ya kanisa weweze kujikinga.

Usharika, kwa kushrikiiana na Dayosisi ya Mashariki na Pwani pia umelazimika kubadili baadhi ya taratibu za ibada ikiwa ni pamoja na washarika kupungiana mikono badala ya kusalimiana kwa kugusana, kupunguza mazoezi ya kwaya kutoka mara mbili kwenda mara moja kwa wiki, kusitisha ibada za jumuiya





(nyumba kwa nyumba) na kusitisha madarasa yote ya kipaimara kwa muda usiojulikana. Pia ibada ya wazee iliyokuwa imepangwa kufanyika tarehe 4 Aprili 2020 sasa imehairishwa mpaka tarehe nyingine itakapotangazwa.

Akizungumza katika ibada ya siku ya Jumapili tarehe 22 Machi 2020 juu ya janga la Corona linaloikabili dunia kwa wakati huu, Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront, Mchungaji Charles Mzinga aliwataka washarika kuendelea kuchukua tahadhari na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Wizara ya Afya ili kujikinga na COVID-19.

Aidha, Mchungaji Mzinga aliwataka washarika kuendelea kujitokeza kanisani ili kumwomba Mungu licha ya hofu iliyotanda mitaani juu ya maambukizi ya virusi vya Corona. "Napenda nitoe wito kwa washarika kujitokeza kanisani kumwomba Mungu ili atunusuru na janga hili huku tukichukua tahadhari zote zinazotolewa na mamlaka husika", alisema Mchungaji Mzinga huku akiongeza kwamba, usharika utandelea kutoa taarifa za mara kwa mara kwa washarika wote juu ya mwenendo wa suala hili, "Kama kutakuwa na mabadiliko mengine yoyote juu namna ya uendeshaji wa shughuli zetu za kila siku hapa usharikani, tutawafahamisha washarika wote haraka iwezekanavyo".

Kupata takwimu na taarifa mbalimbali za kina juu ya virusi vya Corona kwa ulimwengu mzima tembelea; **https://www.who.int/emergencies/diseases/novel-coronavirus-2019**



**TAHADHARI:** Vifaa vyenye maji ya kumiminika pamoja na sabuni vikiwa katika lango kuu la kuingia kanisani, Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront kwa ajili ya washarika kunawa mikono yao kabla ya kuingia ndani ikiwa ni moja ya tahadhari zinazochukuliwa na usharika kupambana na kuenea kwa virusi vya Corona. **Picha: AZF/Paulin Paul**

# Ibada ya Kiingereza sasa inafanyika saa tatu asubuhi ndani ya Kanisa Kuu


**Na Paulin Paul**


Kutokana na mabadiliko ya ratiba za ibada za siku ya Jumapili katika Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront, sasa ibada ya Kiingereza (English Service) inafanyika kuanzia saa tatu kamili asubuhi katika jengo la Kanisa Kuu. Kabla ya mabadiliko haya ambayo yameanza rasmi mwezi Februari 2020, ibada ya Kiingereza ilikuwa ikifanyika kwenye ukumbi wa Mviringo Hall ulioko ndani ya jengo la Luther House kuanzia saa tatu kamili asubuhi.

Kutokana na mabadiliko hayo, ibada ya kwanza ya Kiswahili imebaki kama ilivyokuwa hapo awali ambayo huwa inaanza saa moja kamili asubuhi na ibada ya pili ya Kiswahili kwa sasa inaanza saa nne na nusu asubuhi.

Mabadiliko haya ya ratiba za ibada yamefanyika ili kuwapa fursa kubwa zaidi washarika kuweza kuchagua ni ibada ipi waweze kushiriki kulingana na ratiba za majukumu yao mengine. Hata hivyo, ratiba na shughuli nyingine za katikati ya wiki zinaendelea kubaki kama zilivyo.

Akizungumza katika hatua za mwanzo za kutangaza mabadiliko hayo ya ratiba za ibada, Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront,




Mchungaji Charles Mzinga, alisema kuwa uongozi wa usharika umefikia hatua hiyo ili kutoa fursa pana kwa washarika kuweza kuchagua ibada zinazoendana na muda wanaoupata. "Hapa hatutakuwa tena na kisingizio cha kutokuja kanisani kuabudu kwa kusingizia muda, kama wewe una muda mfupi sana, tumekuwekea ibada ya kiingereza yenye dakika sitini tu, lakini pia kama wewe unachelewa kufika kanisani mapema asubuhi, ibada ya pili ya Kiswahili itakufaa zaidi. Na pia kama wewe unataka umalize ibada mapema ili uendelee na shughuli zako za ujenzi wa taifa, basi ibada ya kwanza ndiyo chaguo lako. Hapa kila mtu anachagua size yake." Mchungaji Mzinga alieleza.

Kwa maelezo na taarifa kwa kina juu ya ratiba na shughuli zote zinazofanyika usharikani, tembelea ofisi ya parish worker au tovuti rasmi ya usharika ***www.azaniafront.org .***




Baadhi ya vitabu vinavyotumika katika ibada ya Kiingereza katika Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront vikiwa tayari kwa ajili ya matumizi. **Picha: AZF/Bertha Semu**

# Faragha ya wazee wa baraza Bagamoyo yafana, wapendekeza ifanyike mara kwa mara



**Na Cuthbert Swai**

Wazee wa baraza 27 wa Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront walifanya faragha (retreat) ya siku mbili kuanzia tarehe 28-29 Feb 2020 wilayanI Bagamoyo katika mkoa wa Pwani ambapo walipata nafasi ya kubadilishana mawazo juu ya masuala mbalimbali yanayohusu usharika na kanisa kwa ujumla.

Faragha hiyo iliyofanyika kwa mafanikio makubwa, ilifanyika katika Hosteli ya Stella Maris na ilifunguliwa na Baba Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa ambaye aliwapongeza wajumbe kwa kuitikia wito wa kuhudhuria na kuwatakia kila la kheri katika kufanikisha lengo la faragha hiyo.

Faragha hiyo ambayo pia ilihudhuriwa na Dean Chidiel Lwiza, ambaye katika siku ya kwanza ya faragha hiyo, alipata fursa ya kuongoza somo lenye kichwa 'Mzee wa kanisa ni nani', somo ambalo lililenga kuwapa mwanga na mwongozo wa kina wazee hao wa baraza ili waendelee kutimiza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa zaidi.





Siku ya pili, Mtumishi Grace Masalakulangwa aliendeleza somo hilo kwa undani zaidi huku akitumia mifano hai, jambo lililowafanya washiriki kuelewa vizuri na kuahidi kuyafanyia kazi mambo yote waliyojifunza.

Katika hatua nyingine, wazee wa baraza walipata nafasi ya kupata mwongozo wa fikra juu ya kupanga mradi wa Kiharaka kutoka kwa mtaalam msanifu wa majengo Dk. Lekule.

Washiriki walifurahia sana jinsi faragha hiyo ilivyoendeshwa na kupendekeza ifanyike mara kwa mara na ikiwezekana kwa siku zaidi ya mbili kutokana na kuwa na umuhimu mkubwa katika kuimarisha utendaji wao wa kazi za kila siku usharikani.



Sehemu ya wazee wa baraza wakifuatilia jambo katika moja ya semina zilizofanyika wakati wa faragha yao iliyofanyika Bagamoyo mkoani Pwani. **Picha: AZF/Cuthbert Swai**



Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront, Charles Mzinga (wa kwanza kulia) akisikiliza kwa makini mjadala uliokuwa unaendelea wakati wa faragha ya wazee wa baraza wa Usharika wa Azaniafront. **Picha: AZF/Cuthbert Swai**

# Wanawake Azaniafront wafanya maombi ya dunia, waombea uchaguzi mkuu Tanzania



**Na Jane Mhina**

'Simama, Jitwike Godoro Lako Uende', hilo lilikuwa ni neno kuu lililotumika kama kichwa cha maombi ya wanawake mwaka huu ambayo yaliadhimishwa duniani kote.

Kila mwaka wanawake wa madhehebu yote ya Kikristo dunian huungana kufanya maombi ya pamoja kumshukuru Mungu kwa ajili ya kuliombea kanisa, kuombea amani katika nchi zao, kuombea familia, wajane na wagane, wazee, watoto, na pia kuombea uchumi katika nchi zao na mwaka huu wanawake wamemwomba Mungu aepushe mbali ugonjwa wa virusi vya corona ambao umeenea katika baadhi ya nchi duniani.

Kila mwaka nchi moja duniani huteuliwa kuandaa neno, kwa mwaka huu, nchi ya Zimbabwe ndiyo iliyoandaa neno kuu lililosema " Simama, jitwike godoro lako uende" neno ambalo linatoka katika kitabu cha Yohana Mtakatifu 5: 8.

Hapa nchini Tanzania, madhehebu ya kikristo hupeana zamu za kuandaa maombi haya, dhehebu la Roman Catholic, ndilo lililokuwa mwenyeji wa maombi haya kwa mwaka huu wa 2020. Maombi haya yalifanyika tarehe 6/3/2020, katika viwanja vya Msimbazi Centre.

Katika ufunguzi wa maombi haya, Askofu Yuda Thadeus Raichi alisema, "Maombi haya ni muhimu kwa sababu yanaimarisha umoja wa makanisa duniani". Pia askofu Raichi aliwaasa wanawake kuwa matendo yao yaendane na maombi hayo ya kumtumaini Mungu kwani ndiye awezaye yote.

"Wanawake waendelee kumwomba na kumtumaini Mungu kwani ndiye pekee anayeweza kusikia sala zetu," askofu Raichi aliwaambia wanawake huku akiongeza kuwa wao ni nguzo na tegemeo katika familia, kanisa, jamii na taifa, pia aliwaomba wanawake waombee uchaguzi mkuu utakaofanyika mwaka huu nchini Tanzania ili uweze kuwa wa amani.

Viongozi kutoka madhehebu mbalimbali ya kikristo walishiriki katika maombi hayo ambapo KKKT Dayosisi ya Mashariki na Pwani iliwakilishwa na Mchungaji Mwangota au Mwanjota ambaye pia ni Katibu wa umoja wa makanisa.

Ubalozi wa Zimbabwe nchini ambao ndio walikuwa waandaji wa neno la maombi, uliwakilishwa na baadhi wa wafanyakazi kutoka ofisi ya ubalozi. Madhehebu yaliyoshiriki katika maombi hayo mwaka huu ni wenyeji Roman Catholic, KKKT, AICT, Baptist, KLPT, Anglican, Life Ministry, Menonite, Methodist, Morovian, Salvation Army na PCEA. Katika maombi hayo, wanawake kutoka usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront pia walihudhuria kwa wingi.





**Katika Picha:** Sehemu ya wanawake kutoka usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront walioshiriki katika maombi ya dunia yaliyofanyika Msimbazi Centre jijini Dar es Salaam. **Picha: AZF/Jane Mhina**

# Azaniafront yaadhimisha siku ya wanawake duniani

**Na Paulin Paul**

Tarehe 8 Machi kila mwaka dunia huwa inaadhimisha sikukuu ya wanawake duniani kama njia mojawapo ya kutambua na kuthamini mchango wa wanawake katika kuleta maendeleo kwenye jamii zao, taifa na dunia nzima kwa ujumla.

Mwaka huu wa 2020, Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront haukuwa nyuma katika kuadhimisha siku hiyo ambapo ibada zote za Jumapili ya siku hiyo ziliongozwa na wanawake huku kichwa cha somo la siku hiyo kikiwa ni "Kataa Ukatili".

Ilikuwa ni siku iliyojaa furaha na mwamko kwani wanawake usharikani ndio walioongoza ibada zote tatu katika siku hiyo, ibada mbili zikiwa ni za Kiswahili na ibada moja ikiwa ni ya Kiingereza. Ibada zote ziliongozwa na wanawake kwa kila huduma, ambapo Zaburi ilisomwa na Mama Erica Malasusa, Litrugia iliongozwa na Bi Lilian Mbowe kwa umahiri mkubwa na Mahubiri yalitolewa na Bi Anna Mzinga aliyewasisitiza wanawake kutumia nafasi zao walizopewa na Mungu katika kuzitumikia jamii zao.


Akihubiri katika ibada zote za lugha ya Kiswahili za siku hiyo, Mama Mchungaji Mzinga, aliwakumbusha wanawake juu ya umuhimu wao katika kuziendeleza famila na jamii zinazowazunguka. Alisema kuwa mwanamke ni nguzo ya familia, hivyo anatakiwa kusimama imara hususani kiroho ili aweze kufanikisha jukumu hilo pevu. "Mwanamke akisimama katika maombi basi familia yake itaponywa, tuna wajibu mkubwa sana wa kuhakikisha familia zetu zinakaa katika mstari ulionyooka machoni kwa Mungu", Mama Mchungaji alisisitiza.

Mbali na huduma za madhabahuni, huduma nyingine zote za siku hiyo kama kusoma matangazo ya usharika na ukusanyaji wa sadaka pia zilisimamiwa na wanawake.

Ibada hizo ambazo pia zilihudhuriwa na Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront, Mchungaji Charles Mzinga, wazee wa baraza pamoja na washarika wote zilifanyika wakati ambapo dunia inapambana kuleta usawa wa kijinsia pamoja na kupunguza changamoto zinazoathiri maendeleo ya wanawake katika nyanja zote za kijamii.









**Katika Picha:** Wanawake wakionekana na nyuso za furaha kwa pamoja mara baada ya kukamilika kwa ibada tatu za siku ya Jumapili tarehe 8 Machi 2020, ambapo zote ziliendeshwa na wanawake kama sehemu ya kuadhimisha siku ya wanawake duniani.

# Wanawake Wafanya Ibada ya Maombi Ya Shukrani

**Na Jane Mhina**

Kila mwaka, katika mwezi wa Januari, wanawake wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani hufanya maombi ya kumshukuru Mungu kwa kuwavusha salama mwaka uliopita na kuwaingiza salama katika mwaka mpya.

Mwaka huu, maombi hayo yalifanyika siku ya Jumamosi, tarehe 25 JanuarI 2020 katika Usharika wa KKKT Segerea ambapo maombi hayo yalibeba neno kutoka katika kitabu cha Zaburi ya 118.1 yaliongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya wanawake na watoto Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Mchungaji Agnes Mangala, ambaye aliwaambia wanawake wamshukuru Mungu kwa maana fadhili zake ni za milele,kwa neema na rehema zake, ametuvusha mwaka salama na kutuingiza mwaka mpya salama.

Kwa upande wake Mchungaji Ismael Mwapile ambaye ni Mchungaji kiongozi wa KKKT Usharika wa Segerea, alifungua maombi hayo kwa kusoma neno kutoka kitabu cha Zaburi 116: 16-19, ambapo aliwaasa wanawake wote waliohudhuria maombi hayo na kuzingatia kuwa, wanawake ni watumishi na daima waendelee kumtolea Mungu dhabihu na kumshukuru Bwana kwa matendo mema mengi anayowatendea katika maisha yao ya kila siku.









Katika Picha: Wanawake wa Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront wakiwa wamejumuika na wenzao wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani walipoungana kushiriki katika maombi ya shukrani yaliyofanyika katika Usharika wa Segerea jijini Dar es Salaam. **Picha: AZF/Jane Mhina**

# Mchungaji Chuwa ahamia Usharika wa Mbezi Beach baada ya kuhudumu Azaniafront kwa miaka kumi

**Na Paulin Paul**

Baada ya kuhudumu kwa takribani miaka kumi katika Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront, Mchungaji Prudence Chuwa sasa amehamishiwa katika usharika jirani wa Mbezi Beach ulioko hapa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika ibada ya Jumapili tarehe 26/01/2020, siku ambayo ilitengwa malum kwa ajili ya washarika wa Azaniafront kumuaga mchungaji wao wa muda mrefu, Mchungaji Chuwa aliwashurkuru washarika wote wa Azaniafront kwa kumpatia ushirikiano uliotukuka katika kipindi chote cha utumishi wake usharikani hapo, alisema ndani ya kipindi cha miaka kumi ameweza kukutana na watu wengi sana na kujifunza mambo mengi.

"Ingawaje nilianzia kuhudumu katika ibada ya Kiingereza lakini pia niliweza kuhudumu katika ibada nyingi sana za Kiswahili, nimefungisha ndoa nyingi hapa na mara kadhaa nimetembelea mitaa inayotunzwa na usharika wa kanisa kuu kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali za kichungaji. Ushrikiano ambao washarika mmenipatia hapa ni wa kiwango cha juu sana, nimeweza kutimiza majukumu yangu bila usumbufu wowote, Mungu awabariki sana", alisema Mchungaji Chuwa.

Kwa upande wake, Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Azaniafront, Mchungaji Charles Mzinga, alimshukuru Mchungaji Chuwa kwa utumishi wake katika usharika wa kanisa kuu na kumtakia kila la kheri katika utumishi wake kwenye usharika wa Mbezi Beach. "Mchungaji Chuwa tumekuwa naye hapa kwa miaka kumi, tumeweza kubarikiwa na utumishi wake hapa. Tunamshukuru sana kwa kazi kubwa ambayo ameifanya na tunamtakia majukumu mema katika kituo chake kipya cha Mbezi Beach, tuna imani atakuwa anakuja kututembelea mara kwa mara maana hapa na Mbezi Beach sio mbali", alisema Mchungaji Mzinga.

Katika ibada hiyo ambayo pia ilihudhuriwa na Askofu wa Dayosisi ya Msahriki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, washarika wote wa AZF walipata fursa ya kuagana na mchungaji wao kwa kumpa mkono wa kheri pamoja na zawadi mbalimbali kwa ajili ya ukumbusho.

Mchungaji Chuwa alianza utumishi wake katika usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront mnamo mwaka 2009 mara tu baada ya kuhitimu mafuzno yake ya kichungaji. Amehudumu katika ibada zote za usharika na kuendesha pamoja na kushiriki katika shughuli mbalimbali za usharika pamoja na Dayosisi ya Mashariki na Pwani.



Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, DK. Alex Malasusa akiwa emeongozana na Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront, Charles Mzinga pamoja na Mchungaji Prudence Chuwa mara baada ya kukamilika ibada ya kwanza usharikani hapo. **Picha: AZF/Paulin Paul**









**Katika Picha:** Mchungaji Prudence chuwa akipeana mikono ya kutakiana heri pamoja na washarika wa Azaniafront mara baada ya kuwaaga washarika hao katika ibada iliyofanyika katika usharika wa Azaniafront. **Picha: AZF/Paulin Paul**

# Habari katika picha



Julai 2019: Mchungaji Prudence Chuwa (kushoto) akitoa historia fupi ya Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront kwa wageni kutoka Marekani waliofanya ziara ya wiki mbili usharikani hapo. **Picha: AZF/Paulin Paul**



Desemba 2018: Mchungaji Prudence Chuwa akihudumu katika ibada ya chakula cha bwana iliyofanyika katika mtaa wa Mvuti, moja ya mitaa inayotunzwa na Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront. **Picha: AZF/Paulin Paul**



Desemba 2018: Mchungaji Prudence Chuwa akifungisha ndoa katika mtaa wa Mvuti. Washarika katika mtaa huu mara zote walikuwa wakifurahia ujio wa Mchungaji Chuwa katika mtaa wao. **Picha: AZF/Paulin Paul**



Desemba 2018: Mchungaji Prudence Chuwa akiendesha ibada ya ubatizo kwa watoto pamoja na watu wazima katika mtaa wa Mvuti. **Picha: AZF/Paulin Paul**



Shamba la mihogo kama linavyoonekana katika eneo la mradi wa Kituo cha Kiroho cha Kiharaka lililopo Bagamoyo moani Pwani. **Picha: AZF/Cuthbert Swai**



Wajumbe wa kamati ya uchumi ya Usharika wa Kanisa Kuu Azaniafront wakikagua shamba la mihogo lililoko Kiharaka. Kama inayoonekana kwenye picha, zao linakaribia kukomaa. **Picha: AZF/Paulin Paul**

# Kwaya ya Agape yazuru Hospitali ya Taifa Muhimbili

**Na Jane Mhina**

Kwaya ya Agape inayohudumu katika ibada ya kwanza siku za Jumapili usharikani Azaniafront, hivi karibuni ilifanya ziara ya uinjilisti katika hospitali ya Muhimbili, kitengo cha mifupa MOI, katika wodi mpya ya watoto ili kuwajulia hali na kuwapa faraja wagonjwa.

Ziara hiyo ya uinjilisti ilifanyika siku ya jumatano tarehe 12 Februari 2020, ililenga kuwasaidia watoto wenye matatizo ya ulemavu wa vichwa vikubwa na ugonjwa wa mdomo wazi. Watoto walipata zawadi kutoka kwa wanakwaya wa kwaya ya Agape pamoja na baadhi ya washarika wa Azaniafront waalioweza kuhudhuria.



Zawadi hizo zilikuwa ni pamoja na bima za afya, juice, maji ya kunywa, biskuti, sabuni, mafuta na dawa za meno. Zawadi hizo ziliwapa faraja na furaha watoto hao ambapo muuguzi katika wodi hiyo,aliwashukuru wanakwaya wa kwaya ya Agape kwa ziara hiyo ya uinjilisti iliyoleta faraja kwa wahitaji. Mungu awabariki washarika wote waliochangia vitu mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia watoto hao.







**Katika Picha:** Wanakwaya wa Kwaya ya Agape wakiongozwa na mwenyekiti wa kwaya hiyo, Ndg Moses Kombe, wakiwa wamejumuika na watoto pamoja na wagonjwa wengine wanaopatiwa matibabu katika hospitali ya Taifa Muhimbili mara baada ya kwaya hiyo kukabidhi msaada wa vitu mbalimbali vya kujikimu wa wagonjwa. **Picha: AZF/Jane Mhina**

# Wanawake Waongoza Ibada ya Kwaresma

**Na Jane Mhina**

Kila mwaka katika taratibu za dhehebu la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), hufanyika ibada za Kwaresma ambazo hufanyika kila siku ya Jumatano kwa muda wa mwezi mmoja kabla ya ibada ya kukumbuka kufa kwa Bwana Yesu Kristo.

Ibada hizi za kipindi cha Kwaresma huwa ni ibada za kujitafakari, kujisafisha na kutubu dhambi kabla ya ibada ya Ijumaa kuu. Mwaka huu wa 2020, ibada hiyo ya Kwaresma iliyokuwa sambamba na ibada ya maombi ya dunia ya wanawake, iliongozwa na wanawake kwa njia ya kutumia kitabu maaluum cha maombi ya dunia ya wanawake.

Ibada hiyo iliongozwa kwa kusoma maneno na mistari ya Biblia yaliyoandaliwa kwenye kitabu hicho, ambayo yalisomwa na wanawake walioandaliwa wakiongozwa na kiongozi wa maombi hayo Mama Veronica Kileo. Pia kulifanyika igizo lililotoka katika kitabu cha Mtakatifu Yohana 5:2-8 lililosema

***'SIMAMA JITWIKE GODORO LAKO UENDE'.***



Wanawake wakishiriki katika igizo kwenye ibada ya Kwaresma iliyofanyika Usharikani Azaniafront, Jumatano tarehe 11 Machi 2020. **Picha: AZF/Jane Mhina**









**Katika Picha:** Wanawake wakisherehesha ibada ya kwaresma kwa kufanya igizo la mateso ya Yesu Kristo ikiwa ni wiki chache kuelekea sikukuu ya Pasaka. **Picha: AZF/Jane Mhina**






# TANGAZA NA KIJARIDA HIKI

Kamati ya Habari na Uhusiano ya Usharika wa Kanisa Kuu la Azaniafront inapenda kuwatangazia washarika wote kuwa inapokea MATANGAZO ya aina mbalimbali (kijamii/biashara) kwa ajili ya kuchapishwa kwenye kijarida hiki kwa gharama nafuu. Hii ni kwa ajili ya washarika tu.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na **Mzee Cuthbert Swai**, Mwenyekiti wa Kamati ya Habari na Uhusiano ya Usharika kwa;

Simu namba: **0763 746 338** au

Barua pepe: **c.swai@yahoo.com**

***Kufahamu zaidi, tafadhali wasiliana na;***

***Pastor Joseph Mlaki***
*Kivukoni Road/Sokoine Drive*
*P.O. Box 71209, Dar es Salaam*
*E-mail: Jmlaki75@gmail.com*
*Mobile: +255 784 708160*